

# »Kufanya kilimo cha mipapai kuwa na faida kwa kiwango kidogo – Sehemu ya 2«

Katika kilimo changamoto mbalimbali hupatikana kama vile wadudu, magonjwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mipapai huzaa matunda mfululizo na huishi kwa miaka 4–5. Mipapai inaweza kutofautishwa tu baada ya kuchanua maua. Mpapai wa kiume hutoa maua mawili na hutoa matunda mwishoni mwa matawi, walakini matunda yake ni ya ubora duni. Mipapai untha hutoa maua ambayo ni ya kiume na ya kike, na yana uwezo wa kujichavusha yenye. Matunda yake ni marefu, nyembamba na ya ubora mzuri.

## Faida za papa

Papai zinaweza kutumika kutengeneza aiskrimu, juisi safi, jamu, jeli, divai, marmalade, peremende n.k.

Papai huzalisha utomvu ambao unaweza kuvunwa na kutumika katika uzalishaji wa papaini. Papain hutumiwa katika viwanda vya pombe, nyama ya makopo na tasnia ya dawa.

Unaweza kufaidika zaidi kuongeza thamani kwa papai.

## Uvunaji wa maji

Wakati wa mvua, vuna maji ambayo yatatumika kumwagilia mazao wakati wa kiangazi. Mwagilia kuwa kutumia njia ya matone ili kuepuka upotevu wa maji.

Bubadilisha mazao ili kuimarisha na kurutubisha udongo. Kilimo mseto kina faida kwa mkulima, kwani hukuruhusu uvunaji mazao tofauti mwaka mzima. Chunguza mazao ili kuangalia kama kuna wadudu na magonjwa. Ikiwa mazao yameshambuliwa, tumia dawa za

kemikali na dawa za majani kudhibiti magonjwa na wadudu.